

# KCSE TRIAL 2020

## KISWAHILI PAPER 3

### SWALI LA KWANZA, SWALI LA LAZIMA

#### SEHEMU YA A: USHAIRI- (Alama 20)

Niokoa muokozi, uniondolee mashaka  
Kuyatukua siwezi, mjayo nimedhikika  
Nimekitiri simanzi, ni katika kuudhika  
Mja wako nasumbuka, nipate niyatakayo

Mja wako nasumbuka, nataka kwao afua  
Nirehemu kwa haraka, nami nipate pumua  
Naomba hisikitika, na mikono hiinua  
Mtenda ndiwe moliwa, nipate niyatakayo

Mtenda ndiwe moliwa, we ndiwe mola wa anga  
Mazito kuyaondoa, pamoja na kuyatenga  
Ukauepusha ukiwa, ya pingu zilonifunya  
Nikundulia muwanga, nipate niyatakayo

Nikundulia muwanga, nipate toka kizani  
Na huzuni n'ondolea, itoke kwangu moyoni  
Mambo mema niegheshea, maovu nisitamani  
Nitendea wa manani, nipate niyatakayo

Igeuze yangunia, dhaifu unipe mema  
Nili katika dunia, kwa afia na uzima  
Moliwa nitimizia, yatimize yawe mema  
Nifurahike mtima, nipate niyatakayo.

## **Maswali**

- (a). Eleza bahari zozote mbili za shairi hili (alama 4)
- (b). Eleza muundo wa shairi hili (Alama 4)
- (c). Mshairi ametumia uhuru wake wa utunzi. Eleza mifano minne huku ukitoa mifano (alama 4)
- (d). Andika ubeti wa pili katika lugha tutumbi (alama 4)
- (e). Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama.2)
- (f). Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi (alama 2)
- (i). Nimedhihika
- (ii). Nifurahike mtima

## **SEHEMU B: RIWAYA – ASSUMPTAMATEI - CHOZI LA HERI**

2. Haki za watoto hazitiliwi maanane katika jamii nyingi za kiasia. Eleza ukweli wa kauli hii kwa kurejelea Riwaya ya chozi la heri (Alama 20)

**au**

3. “Kuukata mkono niliostahili kuubusu yalinifika ya kunifika” (Alama 20)
- a. Eleza muktadha wa dondoo hili (Alama 4)
- b. Eleza namna msemaji alivyokata mkono aliostahili kuuibusu. (alama 6)
- (alama 14)
- c. Eleza tamathali ya usemi unaojitokeza katika dondoo hili. (alama.2)
- d. Fafanua sifa nne za msemaji wa kauli hii (alama 8)

## **SEHEMU C: TATHILIA KIGOGO NA PAULINE KEA**

4. “Na hawa wafadhili wao nao lazima wavunje kambi zao. Sagamoyo twajiweza”
- a. Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
- b. Kwa kutolea mifano saba kwenye tamthilia eleza jinsi kauli hii “Sagamoyo twajiweza” ni kinaya? (alama 14)
- c. Mbali na kinaya tambua mbinu nyingine ya kisanaa katika dondoo hili (alama 2)

**AU**

5. Jadili mbinu wanazotumia wanasagamoyo kujikomboa kutoka utawala dhalimu wa Majoka

(Alama 20)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI - TUMBO LISILOSHIBA**

6. "... Ningeondoka.....mapema niende niibe au niue ili niwe mtu wa maana"

a) Eleza muktadha wa maneno haya (Alama 4)

b) Onyesha vile Kinaya kinavyojitokeza katika dondoo hili (Alama 2)

c) "Kinaya kimetumika kwingine katika hadithi husika. Thibitisha kwa kutumia hoja tisa

(Alama 9)

d). Eleza umuhimu wa msemaji katika hadithi hii (alama.5)

**AU**

7. (a). Eleza namna maudhui ya ndoa yalivyosawiriwa katika hadithi ya Masharti ya Kisasa (alama 13)

(b). Kwa kurejelea hadithi ya Shibe inatumaliza,eleza namna maudhui ya ufiada yanavyojitokeza

(alama 7)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

8 (a) Miviga ni nini? (Alama 2)

(b) Fafanua sifa sita za miviga (Alama 6)

(c) Kwa nini jamii huthamini miviga (Alama 8)

(d). Onyesha udhaifu unaohusishwa na miviga (Alama 4)

